HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 012 | JULAI - SEPTEMBA, 2023

# TUNZA VYANZO VYA MAJI KWA FAIDA YA KIZAZI CHA SASA NA KIJACHO



Ndani:

- ELIMU YA UDHIBITI WA SAUTI ZILIZOZIDI VIWANGO PAMOJA NA MITETEMO YAWA KIVUTIO BANDA LA NEMC MAONESHO YA NANENANE
- UTUNZAJI WA MAZINGIRA NI BIASHARA
- ZIFAHAMU ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI

@nemctanzania NemcTVTanzania

#MazingiraYetuUhaiWetu

www.nemc.or.tz

# YALIYOMO


03 TUNZA VYANZO VYA MAJI KWA FAIDA YA KIZAZI CHA SASA NA KIJACHO

04 USIMAMIZI WA TAKA HATARISHI

05 NEMC YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA WAKULIMA NANENANE - MBEYA

06 ELIMU YA UDHIBITI WA SAUTI ZILIZOZIDI VIWANGO PAMOJA NA MITETEMO YAWA KIVUTIO BANDA LA NEMCMAONESHO YA NANENANE

07 NEMC YASHIRIKI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI KIMKOA

10 DHANA YA UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA MAZINGIRA

11 MKUU WAMKOA WA NJOMBE APONGEZA UTENDAJI KAZI WA MKURUGENZI MKUU NEMC

11 UTUNZAJI WA MAZINGIRA NI BIASHARA

12 VPO NA NEMC WATEKELEZA MRADI WA KUONGEZA UWEZO WA KITAIFA WA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (EMA)

13 NEMC YAWATAKA WAMILIKI WA MABASI KUZINGATIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

14 ZIFAHAMU ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI

15 NEMC YAENDESHA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA MAMLAKA ZA SERIKALI KATIKA MIPAKA


16 RAS IRINGA AITAKA NEMC KUUTAZAMA MTO RUAHA KWA JICHO LA KIPEKEE

17 NEMC KANDA YA KATI YAFANYA ZIARA YA UKAGUZI WA MAZINGIRA MKOANI SINGIDA

17 NEMC YATOA HUDUMA ZA USAJILI WA MIRADI PAMOJA NA WASHAURI ELEKEZI WA MAZINGIRA KWA NJIA YA MTANDAO

18 FAHAMU KUHUSU KATAZO LA VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI

20 KAULI YA MAZINGIRA - KATUNI

## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
**Dkt. Menan Jangu**

**Mhariri Mkuu:**
**Irene John**

**Wachangiaji:**
Dalia Charles
Rose Mtui
Martha Kawishe
Tajiri Kihemba
Nana Elias

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# TUNZA VYANZO VYA MAJI KWA FAIDA YA KIZAZI CHA SASA NA KIJACHO



Maji ni uhai wa kila kiumbe hai kuanzia binadamu, wanyama wa aina zote, viumbe vya baharini na hata mimea kwani viumbe hai vyote uhitaji maji ili viweze kuishi na bila ya maji viumbe hai hukosa uwezo wa kuishi na kwa maana nyingine hufa.

Binadamu tunahitaji maji kwa matumizi mbalimbali ya kila siku kama vile kunywa na shughuli nyingine za nyumbani, lakini pia tunahitaji maji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji kama vile kilimo, viwandani na shughuli za ufugaji wa wanyama.

Licha ya kuwa maji ni uhai wa kila kiumbe hai lakini binadamu ndiye amekuwa kikwazo cha utunzaji endelevu wa maji kwani shughuli mbalimbali zinazofanywa na binaadamu zimekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa vyanzo hivyo vya maji.

Kuna sababu nyingi zinazopelekea uharibifu wa vyanzo vya maji kama vile utekelezaji wa shughuli za kilimo kando ya vyanzo vya maji kama vile mito, mabwawa na chemichemi, ukataji wa miti kwa ajili ya kuni, mkaa na shughuli za ujenzi, uchimbaji wa mchanga na madini mengineyo, shughuli za ujenzi usiozingatia Sheria na taratibu za mipango miji, ufugaji holela kando ya vyanzo vya maji pamoja na utupaji takataka karibu na vyanzo vya maji.

Uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji unapelekea kuwepo na athari nyingi sana zikiwemo kuharibu mfumo wa kiikolojia katika mazingira, kusababisha ongezeko la magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu na magonjwa mengineyo, kusababisha majanga ya mafuriko katika jamii, hukwamisha shughuli za kimaendeleo kama vile kilimo, ufugaji na shughuli nyingine, husababisha kupungua kwa kina cha maji na kupoteza ubora wake lakini pia huchochea uchafuzi wa mazingira kwa kiwango kikubwa.

Kuna mambo mengi ya msingi ambayo yakifanyika yataweza kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji hali itakayopelekea utunzaji wa mazingira yetu kwa ujumla. Mambo hayo ni kama vile jamii kutojishughulisha na kilimo kandokando ya vyanzo vya maji, jamii kutokata miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile matumizi ya kuni, mkaa na shughuli za ujenzi, kutochimba mchanga na madini mengineyo kando ya vyanzo vya maji, kufanya shughuli za ujenzi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za mipango miji, kutojishughulisha na ufugaji holela kando ya vyanzo vya maji lakini pia kutotupa hovyo takataka karibu au kwenye vyanzo vya maji.



Kadiri watu wanavyozidi kuweka makazi yao karibu na vyanzo vya maji na matumizi ya vyanzo vya maji hivyo kuongezeka, kazi ya kuhifadhi vyanzo hivyo pia inazidi kuwa ngumu. Katika sehemu zenye viwanda, maji yanayoweza kutumika kupita kiasi na kuchafuliwa. Lakini watu wa kawaida ambao ndiyo wahitaji zaidi wanaweza kukosa uwezo wa kuzuia tatizo hilo. Matatizo kama haya yanahitaji jamii yote kujipanga na kwa upande wa serikali kuendelea kusimamia Sheria na Kanuni zilizowekwa kuhusiana na Uhifadhi na Utunzaji wa vyanzo vya maji na Mazingira kwa ujumla.

Ni wajibu wa Jamii yote kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na kutunzwa kwa faida ya kizazi cha leo na kizazi kijacho kwani maji ni uhai wa viumbe hai vyote duniani, hivyo bila ya maji hakuna shughuli zinaendelea na hasa uhai wa viumbe hivyo wakiwemo binaadamu huwa mashakani maji yanapokosekana kwani ***"MAJI NI UHAI"***.

# USIMAMIZI WA TAKA HATARISHI




*Mfano wa taka hatarishi*

Taka hatarishi ni taka zozote ambazo ni ngumu na zipo katika mfumo wa kimiminika, gesi na tope (sludge) ambazo kwa sababu ya athari zake kikemikali, kimazingira na katika ustawi wa viumbe hai zinadhuru afya ya binadamu, maisha na Mazingira. Taka hatarishi ni taka zenye tabia zifuatazo: kulipuka, kuwaka moto, ni sumu, zina uwezo wa kuambukiza na uwezo wa kubabua n.k.

Taka hatarishi zipo za aina nyingi zikiwemo madawa ya kilimo, hospitali, mifugo, na viwanda yaliyoisha muda wake, taka za kemikali za majumbani na viwandani, vifaa vilivyochakaa migodini, betri chakavu, mafuta machafu, taka za kielektroniki, taka za mionzi, taka za chuma, matairi chakavu pamoja na taka zote kama zilivyoainishwa katika Kanuni ya 12 ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi, 2021 na Kanuni ya 13 ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za mwaka 2021.

Aidha taka hatarishi zina fursa ya kibiashara kwa ndani na nje ya nchi kutokana na uwezo wake wa kurejelezwa hivyo kusaidia kupunguza athari ya taka hizi katika Mazingira, afya na maisha. Pia kusaidia wananchi kupata kipato kupitia kukusanya, kusafirisha na kuuza taka hizi ndani na nje ya nchi.

Mojawapo ya taka hatarishi ni Vyuma chakavu, viko katika makundi mengi kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi, 2021. Uingizaji wa chuma chakavu unasimamiwa na mkataba wa Bamako kuhusu Uzuiaji wa Uingizaji wa taka hatarishi Barani Afrika wa mwaka 1991 ambao Tanzania ni mwanachama. Mkataba huo umedhibiti uingizaji wa taka hatarishi barani Afrika kutoka nchi ambazo sio mwanachama wa mkataba huu. Waziri anayehusika na Mazingira baada ya kufanya mashauriano na wizara zingine zinazohusika na kwa masilahi ya umma wa Tanzania anaweza kuruhusu kuingiza taka hizo ndani ya nchi ya Tanzania. Kwa muktadha huo vyuma chakavu vinavyoruhusiwa nchini ni vile vinavyotokea ndani ya bara la Afrika na ni nchi mwanachama wa mkataba wa Bamako (1991).

Aidha, kwa Tanzania Bara Taka hatarishi zinasimamiwa na kudhibitiwa na Kifungu cha 133 - 139 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kama ilivyofanyiwa marejeo na (Sheria Na. 3 ya mwaka 2016) ikisomwa pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2021 na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za udhibiti ya usimaimizi wa taka za kielekitroniki za mwaka 2021. Kwa mujibu wa Sheria Waziri mwenye dhamana ya Mazingira ndiye mwenye mamlaka ya kutoa vibali vya kufanya shughuli za kukusanya, kusafirisha, kuhifadhi, na kumiliki au kuendesha kituo au eneo la kurejeleza, kutibu au kutupa taka hatarishi. Kwa muktadha huo NEMC inahusika katika:

a) Kupokea na kuchakata maombi ya vibali vyote vya kuingiza nchini au kusafirisha nje ya nchi taka hatarishi kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba ya kimataifa;

b) Kufanya kaguzi na upelembaji kwa wenye vibali, shehena au sehemu ambazo shughuli za usimamizi wa Taka Hatarishi zinafanyika;

c) Kupokea na kuchakata maombi ya vibali vya usimamizi wa Taka Hatarishi ndani ya nchi ambayo huanzia katika ngazi ya Ofisi za Kanda;

d) Kumshauri waziri kuhusu utoaji wa vibali vya taka hatarishi na taka za kielekitroniki;

e) Kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira fomu za Ufuatiliaji (tracking forms); na

f) Kuanzisha na kudumisha rejista ya taarifa kuhusiana na udhibiti na Usimamizi wa taka hatarishi

NEMC pia inahusika katika kuratibu na kuhakikisha sheria ya Mazingira na Kanuni za taka hatarishi na taka za kielekitroniki zinafuatwa. Hata hivyo, mchakato wa maombi ya vibali umetofautisha kutokana na shughuli za taka hatarishi ndani ya nchi na shughuli zinazohusisha kuingiza, kupitisha au kusafirisha taka hatarishi kutoka/ kwenda nje ya nchi. Kwa shughuli za taka hatarishi ndani ya nchi, mchakato umegawanyika katika makundi makubwa mawili. Kundi la kwanza ni mchakato wa maombi ya vibali kwa wafanyabiashara wadogo wanaotumia vibanda kama sehemu ya kuhifadhia kwa muda na kuajiri vijana wanaopita mitaani na matoroli wakikusanya taka hadi tani 5 au lita 1000 na vijana wanaokusanya taka za kielekitroniki kutoka kwenye makazi, maofisini na viwandani chini ya tani 1. Kundi la pili ni wafanyabiashara wakubwa wanaokusanya taka hatarishi zaidi ya tani 5 kwa lengo la kutumia katika viwanda vya kurejeleza, kusafirisha kwenda nje ya nchi na wanaokusanya kwa ajili ya kuteketeza (incineration).

Kundi la kwanza; mwombaji wa mara ya kwanza anatakiwa ajaze fomu ya maombi Na. 1, awe na leseni ya biashara, cheti cha TIN, Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa mtendaji Kata au Mtaa anapofanyia biashara, taarifa ya ukaguzi kutoka kwa afisa Mazingira, wasifu wa kampuni au biashara na alipe ada ya maombi ya Tshs. 50,000/=. Mwombaji anayehuisha anatakiwa kuwasilisha fomu za ufwatiliaji na taarifa ya kitabibu ya wafanyakazi wanaojihusisha na shughuli za kukusanya na kusafirisha taka hatarishi.

Kundi la pili; mwombaji wa mara ya kwanza wa kibali cha kukusanya, kusafirisha au kuhifadhi taka hatarishi anatakiwa ajaze fomu ya maombi Na. 1 na awe na leseni ya biashara, cheti cha incooperation na Memorandum and Article of Association kama ni kampuni, cheti cha TIN, wasifu wa biashara au kampuni na alipe ada ya maombi ya Tshs. 50,000/= kwa kila kibali anachoomba. Mwombaji anayehuisha anatakiwa kuwasilisha fomu za ufwatiliaji (tracking form) na taarifa ya kitabibu ya wafanyakazi wanaojihusisha na shughuli za kukusanya na

Inaendelea Uk. 06

# NEMC YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA WAKULIMA NANENANE - MBEYA




*Viongozi wa Dini, Vyama na Serikali wakifuatilia Hotuba ya Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Ufunguzi wa Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limeshiriki maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane Jijini Mbeya kwa lengo la kutoa elimu ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake kwa wananchi na Taasisi mbalimbali zilizoshirki.

Maonesho hayo yaliyofunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango yenye kauli mbiu isemayo; **"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula"** na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa vyama na Serikali, akiwemo Naibu Waziri wa mifugo na uvuvi, Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa wabunge, Waheshimiwa Madiwani, Mameya wa jiji la Mbeya, Balozi wa Namibia nchini, Wakuu wa Taasisi, wadhamini, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini na vyama vya kimila, wakuu wa Wilaya na wakulima yamelenga kukumbusha umma wa watanzania umuhimu wa kuthamini mchango mkubwa wa vijana na wanawake na shughuli za maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi kwani katika uhalisia wake vijana na wanawake ndio wanaochangia nguvu kubwa ya uzalishaji, uchakataji, usambazaji na uuzaji wa chakula katika masoko ya ndani na nje ya Nchi.

Amesema maonesho haya pia ni maandalizi ya kuelekea mkutano wa jukwaa la mifumo ya chakula Afrika (Africa Food Forum) unaotarajiwa kufanyika septemba 5 hadi 8 mwaka huu Jijini Dar es salam na kuwasihi vijana kushiriki ili kupata mbinu za kisasa za ufanyaji wa kilimo mifugo na uvuvi kwani ndio nguzo pekee inayolihakikishia Taifa usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwanda, ajira, kipato na kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni na hivyo kukuza uchumi wa Nchi yetu kwa ujumla.

"Serikali imedhamiria kuongeza uzalishaji, tija na thamani katika mazao yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwekeza katika sekta hiyo, kwani ndio sekta pekee yenye uwezo wa kutoa ajira kwa vijana na itakayoweza kuwaongezea kipato na kukuza uchumi, ni kwa sababu hiyo bajeti ya Wizara imeongezwa kufikia bilioni 295 kwa mwaka 2023/2024 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 330%"

*Inaendelea Uk. 08*

# ELIMU YA UDHIBITI WA SAUTI ZILIZOZIDI VIWANGO NA MITETEMO YAWA KIVUTIO BANDA LA NEMC MAONESHO YA NANENANE



Elimu ya Udhibiti wa sauti zilizozidi viwango na mitetemo kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake, yavutia wadau wengi hasa ikizingatiwa ndio changamoto kubwa inayoikumba jamii kwa sasa.

Elimu hiyo iliyohusisha tafsiri ya kawaida ya sauti zilizozidi viwango, vyanzo vya sauti zilizozidi viwango, athari za sauti zilizozidi viwango pamoja na njia za kudhibiti sauti zilizozidi viwango na mitetemo imewafurahisha wengi hasa wale waliozungukwa na nyumba za ibada, viwanda na kumbi za burudani.

Akizungumza na wadau hao Bi.Furaha Benjamin ambaye ni Afisa Mazingira NEMC, Kanda ya Nyanda za Juu kusini amesema elimu hii ni vizuri kuifahamu kwa usahihi ili mmiliki wa kumbi au kiwanda au wale waliozungukwa na vyanzo vya kelele wajue namna sahihi ya kudhibiti kwa mstakabali wa Afya.

Bi Furaha amezitaja athari za sauti zilizozidi viwango kuwa ni wanafunzi kushindwa kujisomea, husababisha ulemavu wa usikivu, kuharibu mahusiano ya jamii, kukosa usingizi, huathiri mawasiliano pamoja na kukosesha wagonjwa na wazee usingizi.

Ameziainisha njia za kuzuia sauti zilizozidi viwango ambazo husababisha kelele kuwa ni matumizi sahihi ya ardhi kwa ajili ya shughuli zinazozalisha kelele, wamiliki wa biashara kupata vibali kutoka mamlaka husika pamoja na matumizi ya vidhibiti sauti.

Wananchi na wadau wengi waliomiminika katika Banda la NEMC maonesho ya Nanenane Mjini Mbeya, wamefurahishwa na elimu ya udhibiti wa sauti zilizozidi viwango na mitetemo inayotolewa.

*Inatoka Uk. 04*

## USIMAMIZI WA TAKA ...

kusafirisha taka hatarishi.

- Iwapo mwombaji anaomba kibali cha kusafirisha taka hatarishi nyaraka zinazoongezeka ni maelezo ya mfumo wa usafirshaji utakao tumika kusafirisha taka hatarishi.
- Iwapo mwombaji anaomba kibali cha kuhifadhi taka hatarishi nyaraka zinazoongezeka ni cheti cha Tathmini ya athari ya Mazingira (TAM) au cheti cha ukaguzi wa Mazingira, na mpango wa dharura wa eneo la kuhifadhi.
- Iwapo mwombaji anaomba kibali cha kumiliki au kuendesha mtambo au eneo la kurejeleza, kutibu au kutupa taka hatarishi nyaraka zinazoongezeka ni cheti cha Tathmini ya athari kwa Mazingira (TAM) au cheti cha ukaguzi wa Mazingira, nyaraka za umiliki wa ardhi au kithibitisho cha kupanga eneo pamoja na mpango wa matumizi ya ardhi, mpango wa nishati (energy plan) wa eneo la kutibu au kutupa taka hatarishi, maelezo ya mtambo wa kutibu au eneo la kutupa taka hatarishi, mpango wa dharura, na vibali husika kutoka mamlaka zingine.

Kwa shughuli za taka hatarishi zinazohusisha kuingiza, kupitisha au kusafirisha taka hatarishi kutoka/ kwenda nje ya nchi maombi yanahusisha kupata ridhaa kutoka nchi taka hatarishi zinakopelekwa au zinakotokea.

Kibali kinapotolewa na Mh. Waziri mwenye dhamana ya Mazingira huja na masharti ya jumla. Masharti haya yanatoa mwongozo wa kufanya biashara hii bila kuathiri Mazingira, afya ya binadamu, pamoja na jamii kwa ujumla. Pia adhabu hutolewa kwa wanaoikiuka Sheria katika biashara hii na adhabu hizo ni pamoja na kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano au isiyozidi shilingi billion kumi au kifungo kisichozidi miaka kumi na miwili au vyote.

Zipo changamoto ambazo NEMC hukutana nazo katika usimamizi wa taka hatarishi hususani vyuma chakavu ni pamoja na wizi na uharibifu wa miundombinu unaosababisha athari za kiuchumi, kijamii na kimazingira. Pia wizi wa vifaa vya nyumbani na magari ambazo huweza kuuzwa kama vyuma chakavu, Elimu na uelewa mdogo wa wadau kuhusu udhibiti na Usimamizi wa taka hatarishi, matumizi ya lugha ya kiingereza imekuwa changamoto kwa wadau kuelewa matakwa ya kisheria, kikanuni na kufwata masharti ya vibali pamoja na Wafanyabiashara kutokumalizia au kutofanya mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira au ukaguzi wa Mazingira katika maeneo yao.

# NEMC YASHIRIKI KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI - KIMKOA




*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watendaji wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na NEMC katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mwinjuma, Makumbusho Jijini Dar es Salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limeshiriki maadhimisho ya Mazingira Duniani, yaliyofanyika Kimkoa katika viwanja vya Mwinjuma vilivyopo Kata ya Makumbusho Manispaa ya Kinondoni na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa vyama na Serikali.

Akiongea katika Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu isemayo "Pinga uchafuzi wa Mazingira utokanao na mifuko ya plastiki" mgeni rasmi ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila amesema, Mkoa wake unaungana na wadau wa Mazingira pamoja na wananchi kote dunani kuiadhimisha siku hii muhimu ya Mazingira kwa kaulimbiu thabiti yenye kuweka mkazo matumizi sahihi ya vifungashio na sio mifuko ya plastiki kama vibebeo ili kutunza mazingira.

Ameongeza kuwa kauli mbiu hii inatoa chagizo kwa kila mwananchi katika Mkoa wake kuelewa maana halisi ya kuhifadhi mazingira na kuachana na matumizi ya mfuko ya plastiki iliyokatazwa kwa mujibu wa Kanuni za mwaka 2019 na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali namba 304.

"Mkoa wa Dar es salaam ni Jiji la biashara, hivyo uchafuzi wa mazingira kwa mifuko ya plastiki umekuwa dhahiri kabisa, na hii inatokana na uwepo wa viwanda bubu vingi, lakini pia Mkoa wangu umekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza katazo hili la mifuko ya plastiki kwa kushirikiana na NEMC pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa hivyo jitihada ni kubwa lakini hazitoshi bila nyie wananchi wenzangu kutuunga mkono" alisema Albert Chalamila.

Naye Bi Glory Kombe, Meneja wa Kanda, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu NEMC amesema wajibu ilionao Taasisi yake ni kuishauri Serikali katika masuala ya Mazingira, lakini pia ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya waka 2004 na Kanuni zake na kwamba imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha agizo la Serikali la kutokomeza mifuko ya plastiki linatekelezwa kwa weledi na kwa wakati.

Amesema NEMC inaendelea kutoa elimu ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira, lakini pia inaendelea kufanya kaguzi mbalimbali kwenye viwanda na masoko, huku ikihakikisha viwanda bubu vinadhibitiwa kwa mujibu wa Sheria.

Maadhimisho hayo yaliyosheheni burudani mbalimbali yamehudhuriwa pia na viongozi wa vyama na Serikali, Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es salaa, TFS, pamoja na wadau wa Mazingira.

Inatoka Uk. 05

# NEMC YASHIRIKI MAONESHO ...

Amesema Dkt. Mpango

Aidha ameyataja malengo mengine ya ongezeko la bajeti hiyo kwenye sekta husika kuwa ni kuimarisha maeneo ya huduma za utafiti na ugani, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi, kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo, kuendeleza kilimo umwagiliaji, kuimarisha upatikanaji wa mitaji pamoja na kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kilimo, kuimarisha mitaji, kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo na mifugo, na kuhamasisha uanzishwaji wa kilimo cha umwagiliaji.

Amehimiza wananchi wa Mkoa Ruvuma na Nyanda za juu kusini kutembelea maonesho haya kwani watapata fursa ya kujifunza matumizi mbalimbali ya mbolea na viuatilifu katika sekta hizi kwa ajili ya maendeleo yao na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa mpango amesisistiza yafuatayo:-

- Maonesho haya ni kwa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi hivyo ni muhimu wapate fursa ya mabanda yao kutembelewa na viongozi.




- Kuanzia sasa wananchi waingie kwenye viwanja vya maonesho ya Nanenane bila kulipa, vinginevyo lengo la kutumia fursa hii kwa wananchi wa kawaida halitatimia.
- Kuanzia mwakani ni vema tuanze kualika Nchi nyingine waje kushiriki maonesho ya Nanenane
- Tunataka riba ya kukopeshwa kwa wakulima wetu ishushwe zaidi.
- Waziri mwenye dhamana ya kilimo akae na Waziri wa fedha kuangalia namna wezeshi ya kanzisha mfuko wa maendeleo wa kilimo (Agricultural Development fund) ili usaidie kupunguza riba za mikopo itokayo kwenye mabenki.
- Pongezi nyingi ziende kwa watafiti na wagunduzi wetu kwa kufanya kazi kubwa katika sekta muhimu kama hii na zoezi hili liambatane na kuwapatia hakimiliki.




Naye Waziri wa Kilimo na Uvuvi Mhe. Hussein Bashe alipozungumza amesema kufuatia maelekezo yaliyotolewa mwaka jana ya kuvifanya viwanja vya John Mwakangale Mbeya na Dodoma kuwa vya kudumu kwa maonesho pamoja na kualika Mataifa mbalimbali kushiriki maonesho yametekelezwa kwa kutenga bajeti itakayoboresha kwa kiwango cha kimataifa na kuzinduliwa na Mhe. Rais mara baada ya kukamilika.

Amesema viwanja hivyo vitaboreshwa kwa kiwango cha kimataifa kitakachowezesha shughuli hizo kuendelea kwa mwaka mzima na kuwapatia wananchi fursa ya kuendelea kutangaza biashara zao.

"Mhe Makamu wa Rais mwaka jana mlitupa maelekezo kwamba Tanzania tubadili mfumo wetu wa maonesho wa Nanenane katika viwanja hivi vya John Mwakangale na tuweze kuufanya kuwa ni wa

kudumu, napenda kukupa taarifa ya kwamba katika viwanja ambavyo vitakuwa vya kudumu kwenye nyanda za juu kusini, kiwanja mojawapo ni kiwanja cha Mbeya, lakini katika bajeti mmetupitishia fedha tayari, hivyo tutaanza marekebisho yake kuanzia mwaka huu wa fedha ili kiweze kuwa na hadhi ya Kimataifa kwa ajili ya maonesho na kuanzia mwaka kesho tutaalika viongozi wote wa Nchi za Afrika kushiriki maonesho'' Amesema Bashe.

Ameeleza kuwa kiwanja kingine kitakachofanyiwa maboresho kwa hadhi ya kimataifa ni kiwanja cha Dodoma ambapo kitakuwa na miundombinu yote itakayohusisha maeneo maalumu kwa wenzetu wa nchi za Afrika pamoja na wakulima watakaoambatana nao na bidhaa kufanya maonesho kwani ndio fursa pekee ya kujitangaza kimataifa.

Akiendelea kufafanua amesema Serikali ya awamu ya sita imeipa kipaumbele sekta ya kilimo mifugo na uvuvi kwa kuhakikisha inaboresho miundombinu pamoja na pembejeo za kilimo, hali iliyopelekea uzalishwaji kwa kipindi cha mwaka 2023 kufikia tani milioni 20 kutoka tani milioni 17 zilizozalishwa msimu uliopita.

Ameahidi kusimamia mikakati iliyopo kwenye Wizara husika ili kufikia malengo chanya ya uzalishwaji kama vile kufufua kampuni ya mbolea ya TFC na kushirikiana nao katika kuboresha pembejeo za mazao ya kilimo na mifugo, kujenga mabwawa makubwa 100 kwa ajili ya kurahisisha umwagiliaji na kuwataka wananchi kuheshimu vituo vya utafiti kwani kuvivamia ni kuhatarisha usalama wa wananchi kwa kizazi cha leo na kesho.

Nalo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kama mdau wa mazingira limeshiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Kilimo kwa lengo la kutoa elimu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira kwa wadau wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake. Baraza katika maonesho hayo limetekeleza jukumu la

i. Kusajili washauri elekezi wa Mazingira pamoja na miradi kwa njia ya mtandao;

ii. Kupokea maoni, ushauri na malamiko kutoka kwa wadau mbalimbali pamoja na kuyafanyia kazi;

iii. Kuikumbusha jamii umuhimu wa kutunza na kuhifadhi Mazingira kwa kuzingatia matumizi sahihi ya vifungashio, umuhimu wa udhibiti wa sauti zilizozidi viwango, umuhimu wa kufanya Tathimini ya Athari kwa Mazingira; na

iv. Kuihamasisha jamii (Wanafunzi) umuhimu wa uanzishwaji wa klabu za Mazingira Mashuleni na vyuoni kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Nchi yetu.

Katika hatua nyingine Baraza kupitia wataalamu wake kwa muda wa siku tisa, walielimisha wadau wa kilimo, mifugo, uvuvi na jamii kwa ujumla umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji, umuhimu wa matumizi ya mifuko mbadala, umuhimu wa kuwa na kilimo endelevu kwa kupunguza matumizi ya kemikali/viuatilifu vinavyoathiri Mazingira, umuhimu wa kudhibiti sauti zilizozidi viwango, umuhimu wa kusajili miradi kwa njia ya kielektroniki pamoja na umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kabla ya Mradi kuanzishwa. Washiriki pia walielimisha wanafunzi wa shule za Msingi, Sekondari na vyuo umuhimu wa kuanzisha Klabu za Mazingira Mashuleni na Vyuoni.

Pamoja na kutoa elimu ya Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake, Baraza pia limepokea ushauri na malalamiko yanayohusiana na sauti zilizozidi viwango, gharama za kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira, utiririshaji wa maji taka, elimu ya Mazingira kutokufika vijijini, matumizi holela ya viuatilifu, matamko ya kisiasa kukinzana na Sheria ya Mazingira, ukataji holela wa miti, usimamizi mbovu wa taka ngumu, kutokuwepo kwa muongozo wa uandaaji wa taarifa za mwaka za Mazingira na kutumwa Halmashauri ili Afisa Mazingira wa Halmashauri awasilishe Baraza ili kupunguza gharama, kutokuwepo kwa alama zilizoandaliwa na Baraza zitakazoonesha maonyo ya uhatarishi wa uchafuzi wa Mazingira, kutokuwepo na Mfumo wa kielektroniki wa kumtambua Mwekezaji ameshapata cheti cha Mazingira.



*Washiriki wa Baraza wakipokea maoni kutoka mwananchi (kushoto) na kulia ni Mhe. Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Njombe*

# DHANA YA UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA MAZINGIRA



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis akikagua ukuaji wa mti uliopandwa katika Barabara ya Ihumwa wakati wa ziara ya kukagua zoezi la upandaji miti jijini Dodoma.*

Kwa miaka mingi duniani kote Sheria za Mazingira zimekuwa zikitumiwa na Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na mifumo ya hewa, maji, viumbe hai, udongo na afya ya jamii. Hali kadhalika, Tanzania pia imekuwa ikitumia Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 kuzuia uchafuzi wa mazingira, kulinda mimea na viumbe hai, kuzuia utupaji wa taka hatarishi na kemikali, kuzuia uchafuzi wa hewa, kelele na mitetemo. Aidha, utekelezaji wa sheria hii umesaidia kuzuia utiririshaji wa majitaka kwenye mazingira na kuhakikisha vyanzo vya maji vinaendelea kuwa safi na salama kwa afya ya jamii na mazingira kwa ujumla.

Hata hivyo, kuwa na Sheria ya mazingira pekee haitoshi kupunguza changamoto hizi za kimazingira zinazojitokeza. Ndio maana lazima Serikali ihakikishe kuwa shughuli za kijamii zinafanywa kwa kuzingatia matakwa ya Kisheria yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake. Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) inasimamia mikakati yote endelevu ya kuhimiza na kufuatilia shughuli za uchafuzi kwa kuzingatia viwango vya kimazingira vinavyotakiwa. Hivyo, makala hii inatoa muhtasari wa msingi wa dhana zinazopelekea kuwa na mafanikio ya utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira.

Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ni sehemu ya mpango endelevu wa shughuli za Baraza za kila siku katika kuhifadhi na kusimamia mazingira kwa ujumla. Mpango huu unaanza pale ambapo umma unatambua kuwa kuna shida ya kimazingira na Serikali kuchukua hatua stahiki katika kushughulikia shida hizo. Serikali imeandaa Sheria na Kanuni za kuweza kutatua shida na changamoto za kimazingira lakini pia Baraza huandaa mpango wa kuweza kufikia malengo ya usimamizi wa Sheria na kanuni hizi. Ufuatiliaji na utekelezaji wa Sheria unafanywa kwa kuzingatia misingi ya Sheria ya usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa jamii inazingatia matakwa ya Kisheria. Baraza limelipa kipaumbele suala la Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sheria na kuhakikisha linakuwa endelevu kwa kujitathmini na kufanya marekebisho ya mara kwa mara ili kuboresha shughuli zake na kuhakikisha shughuli za jamii zinakuwa endelevu.

Baraza linatambua kuwa utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi, hivyo Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ili uwe endelevu unaanza kwa kuhakikisha kuwa jamii husika zimepewa elimu ya kutambua matatizo na changamoto za kimazingira zinazoweza kujitokeza katika maeneo yao. Miradi ya maendeleo na shughuli za kibinadamu zinapitia michakato ya Kisheria ya kutatua matatizo ya kimazingira ikiwa ni pamoja na kufanya Thathmini za Athari kwa Mazingira (TAM) na kufuata mifumo mbalimbali ya utunzaji na usimamizi wa mazingira. Mifumo ya utunzaji wa mazingira mara nyingi hufuatwa na wawekezaji kwa sababu wengine ni wadau wa kutunza mazingira, au mahitaji ya kibiashara na utii wa Sheria kama inavyotaka. Hivyo ni muhimu kujua aina ya wawekezaji wetu ili kuweza kusaidia kila mmoja kwa namna ya uwekezaji wake.


Ufuatiliaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira una manufaa kwa jamii, Umma na wawekezaji. Hii inaonyesha jamii inatekeleza Sheria ya Mazingira kupitia utawala bora wenye kuleta usawa kwa wawekezaji wote. Lakini pia inaonyesha uimara wa taasisi kama chombo cha Kitaifa ambacho kimepewa dhamana ya kusimamia mazingira ili umma uendelee kunufaika na huduma zitokanazo na mifumo ya Kiikolojia na kulinda afya ya jamii. Hata hivyo, kwa wawekezaji hii inawapa motisha wa kuwekeza kwani hupunguza vihatarishi katika biashara zao kwa kuwa wabunifu zaidi na kuongeza ushindani unaotengeneza bidhaa bora na ajira endelevu.

Sheria ya mazingira imeweka mfumo wa utekelezaji wa Sheria kwa kutambua kuwa shughuli za maendeleo lazima ziwe endelevu, hivyo uchafu wa taka unaorudi katika mazingira lazima uwe katika kiwango kinachokubalika kwa kutoathiri mifumo ikolojia, viumbe na afya ya jamii. Kuna viwango vya uchafuzi katika maji, kelele, udongo na hewa ambavyo shughuli za maendeleo lazima zizingatie ili kutoharibu mazingira. Pale ambapo uwekezaji umefanyika kwa kuzingatia matakwa yote na miundominu sahihi imetumika, ni wazi kuwa viwango vya kimazingira vinafikiwa katika uwekezaji wa aina zote. Pale ambapo viwango vinashidwa kufikiwa, Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inatoa uzingatiaji kwa kutumia hatua ambazo ni onyo, faini, kufunga au kuchukua hatua za kufungua mashtaka.

Ili kuhakikisha mpango endelevu wa uzingatiaji wa Sheria ya mazingira ya mwaka 2004, mwekezaji anapaswa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla hajawekeza. Hivyo mpango wa utunzaji wa mazingira utazingatiwa wakati wa ujenzi na uzalishaji/uendeshaji wa mradi. Sheria pia inasisitiza kuwa, baada ya kuanza kufanya uzalishaji, mwekezaji lazima azingatie kufanya ufuatiliaji wa viwango vilivyowekwa kwenye mpango na kila mwaka aweze kuandaa taarifa ya kila mwaka ya kimazingira na kuiwasilisha Baraza. Jamii inajukumu la kutoa taarifa pale ambapo kunakuwa na hali ya uchafuzi wa mazingira. Vilevile, Baraza limejiwekea utaratibu wa kukagua athari za mazingira katika shughuli za kimaendeleo ili kuweza kusaidia kukidhi matakwa ya Sheria ya Mazingira.

Pamoja na hatua zote hizi, bado hakuna Uzingatiaji na Utekelezaji thabiti wa Sheria ya Mazingira. Hivyo Baraza linatoa rai kwa jamii, wawekezaji na mamlaka nyingine zote kushiriki katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa faida ya kizazi hiki na kijacho.

# MKUU WA MKOA WA NJOMBE APONGEZA UTENDAJI KAZI WA MKURUGENZI MKUU NEMC




*Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka*

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka amempongeza Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka kwa utendaji wake mzuri wa kazi hasa kwenye masuala ya usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

Amesema kwa uwajibikaji wake huo umesaidia kupunguza malalamiko mengi yahusuyo mazingira na utekelezaji wa miradi hali iliyowezesha uwekezaji kukua kwa kiwango kusudiwa katika Nchi yetu.

"Nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Gwamaka kwa namna ambavyo ameisimamia Taasisi kwa kupunguza malalamiko mengi hasa kwa kuanzisha Ofisi za Kanda ambazo sasa zimepunguza gharama kwa wadau kupata huduma, lakini pia tunampongeza kwa kuendelea kutoa elimu kabla ya adhabu katika masuala ya Mazingira" Amesema Mhe. Mtaka.

Ameongeza kuwa kwa NEMC kuanzisha ofisi za Kanda kwa Nchi nzima ni uzalendo wenye tija kwani imesogeza huduma kwa wadau hali iliyopelekea kupunguza gharama kwa wadau hasa wawekezaji katika upatikanaji wa huduma.

# UTUNZAJI WA MAZINGIRA NI BIASHARA

Ni kauli yake Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka alipozuru Banda la NEMC katika Maonesho ya Nanenane kupata elimu ya Utunzaji na Uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

Amesema Utunzaji wa mazingira ni faida na mazingira ni maisha ya kila siku anayoishi mwanadamu hivyo kuyapendezesha kwa kupanda miti yenye faida au ukoka kwa ajili ya biashara ni jambo jema linalotakiwa kuzingatiwa.

"Leo mazingira ni biashara, na ndio maana tunafanya kampeni ya hewa ukaa, mazingira leo hata ukipanda ukoka mtu anakuja anataka umuuzie, leo hakuna mti ambao sio biashara, leo hata mtu akipanda miti mizuri anapata wateja, maana wajenzi wapya siku hizi wanahitaji vitu vizuri kwa ajili ya urembo." Amesema Mhe. Mtaka.

Ameongeza kuwa ni vema wananchi wakatumia fursa za maeneo ambayo hali ya hewa inaruhusu kupanda miti yenye faida wakafanya hivyo ili kutunza mazingira na kufanya biashara pia.

Amezitaja faida za kutunza mazingira kuwa ni kupata hewa safi, tunapata dawa na chakula, tunapunguza hewa ukaa, tunapata vifaa kwa ajili ya ujenzi, tunakuwa na afya njema, tunapata maji safi na salama ya kutosha.



# VPO NA NEMC WATEKELEZA MRADI WA KUONGEZA UWEZO WA KITAIFA WA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (EMA)




*Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira NEMC Dkt. Menan Jangu akifafanua jambo wakati wa mafunzo kwa watumishi wa mipaka ya Namanga na Holili/Taveta Jijini Arusha.*

Ofisi ya Makamu wa Rais (VPO),) kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) zinatekeleza mradi wa miaka mitatu (3) wa "Kuongeza Uwezo wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira". Mradi huo umefadhiliwa na Serikali ya Uswidi. Lengo kuu la mradi ni kuongeza uwezo wa kitaifa wa kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ya usimamizi endelevu wa mazingira nchini Tanzania. Mradi huu unatarajiwa kutoa elimu juu ya usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa Taasisi za serikali na vyombo muhimu vya kisheria, kutoa vifaa na maarifa ya kusaidia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uboreshaji wa usimamizi wa mazingira nchini Tanzania.

Mradi huu ni muhimu kwani utaleta tija katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 20 ya mwaka 2004, inayotoa muongozo wa utawala na mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira ambao unapita katika ngazi zote za utawala wa Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sheria ya Mazingira inaeleza zaidi zana mbalimbali za usimamizi wa mazingira kama vile Tathmini ya Mazingira, Viwango vya Mazingira na vyombo vya kiuchumi. Aidha, Sheria inatoa masharti ya maendeleo na utangazaji wa Kanuni, Miongozo na utekelezaji wa Sheria kwa ufanisi.

Sababu kubwa ya kuanzisha mradi huu ni kuwepo kwa changamoto miongoni mwa Taasisi na wadau mbalimbali katika kukidhi vigezo vya kimazingira kwa mujibu wa Sheria wanapotekeleza miradi na shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Hali hii inajitokeza kwa sababu ya uwezo duni wa kitaasisi kutekeleza Sheria ya Mazingira, na kiwango cha chini cha uelewa wa umma juu ya majukumu yao katika kuitekeleza Sheria ya Usimamizi Mazingira.

## MALENGO MAHUSUSI YA MRADI

Mradi huu unalenga kuongeza uwezo wa kitaifa wa kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa usimamizi uendelevu wa mazingira nchini Tanzania, mradi utarahisisha uundaji wa Kanuni, miongozo na zana zingine za vitendo kwa matumizi endelevu ya maliasili. Zaidi ya hayo, mradi utaanzisha mfumo wa wa utoaji wa leseni za mazingira kwa njia ya mtandao na vibali, ufuatiliaji na tathmini na kushughulikia malalamiko. Zaidi ya hayo, mradi utarahisisha utendaji kazi wa Taifa Mfuko wa Dhamana ya Mazingira na utoaji wa vifaa vya ufuatiliaji na utekelezaji wa

## MAENEO MAALUMU YALIYOLENGWA NA MRADI

Mradi umelenga katika maeneo muhimu matano ambayo yataimarisha zaidi utekelezaji wa EMA. Maeneo hayo ni kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria kwa usimamizi madhubuti wa mazingira, kuboresha utoaji wa leseni za mazingira na kujenga uwezo wa ufuatiliaji, kuimarisha uwezo wa kimkakati wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, kuongeza uwezo wa Wizara za Serikali, Idara na Wakala (MDAs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) wa kutekeleza ipasavyo Sheria ya Mazingira na kuwezesha ufanisi mawasiliano kwa umma na ushirikishwaji wa kimkakati wa wadau maalumu.

### Shughuli za mradi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2022/2023

Kulingana na mpango kazi wa utekelezaji wa mradi kwa mwaka fedha 2022/2013 NEMC ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo; Kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria kwa ajili ya usimamizi bora wa mazingira kwa kuendesha mafunzo maalumu juu ya Usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa Mamlaka zinazosimamia mipaka ya Nchi. Pia kutoa mafunzo juu ya ukaguzi na udhibiti wa bidhaa zinazogusa uchafuzi wa mazingira Taasisi nyingine za Serikali kama TRA,TBS, Wizara ya Afya na Kilimo. Kuboresha mfumo wa kutoa leseni za mazingira na kufanya ufuatiliaji kwa kuanzisha kanzidata juu ya usimamizi na udhiti wa takataka nchini. Kuzijengea uwezo Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa juu ya utekelezaji bora wa Sheria ya Mazingira kwa kutoa mafunzo maalum kuhusu zana za usimamizi wa mazingira.

### Shughuli za mradi zilizopangwa ambazo zimeshatekelezwa mpaka sasa

Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2023 Baraza la Taifa la Hifadhi na

*Inaendelea Uk. 15*

# NEMC YAWATAKA WAMILIKI WA MABASI KUZINGATIA UTUNZAJI WA MAZINGIRA



Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limewataka wamiliki wa mabasi kuzingatia Utunzaji na Uhifadhi wa mazingira kwa kuweka vyoo na vitenganishi taka kwenye mabasi yao wanapokuwa safarini.

Agizo hilo limetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Samuel Mafwenga Gwamaka alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukithiri kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na abiria kwenye mabasi pamoja na namna sahihi ya kudhibiti uchafuzi huo katika mkutano uliofanyika Ukumbi wa NEMC Dar es aalaam

Amesema abiria wa mabasi wamekuwa chanzo kikubwa cha uchafuzi wa mazingira kwa kutupa taka madirishani na kuchimba dawa wakati wa safari ndefu hali inayopelekea kuhatarisha maisha yao pamoja na kuchafua mazingira

"Kumekuwa na tabia ya abiria kutupa mabaki ya vyakula madirishani popote pale, au kwenda haja kubwa na ndogo wakati wa safari ndefu barabarani, huko kuna hifadhi za misitu, kuna mbuga za wanyama kuna hifadhi za barbara zote hizi zinatakiwa kulindwa, kwa maana hiyo hii sio tabia sahihi kwanza ni kuchafua mazingira, lakini pia ni kuathiri afya, na kubwa zaidi ni kudhalilisha wanawake" amesema Dkt. Gwamaka.

Ameongeza kuwa mabasi yote ya abiria wa safari ndefu yanapaswa kuzingatia Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa kuweka vyoo na vitenganishi vya taka kwenye mabasi hali itakayosaidia kuepuka uchafuzi wa mazingira.

Amesisitiza kuwa uchafuzi wa aina hii una athari kubwa katika mazingira kwani huibua magonjwa ya mlipuko, husababisha kuchafuliwa na kuziba kwa vyanzo vya maji hupelekea mikondo ya maji kuziba, husababisha mchafuko wa hali ya hewa pamoja na kuharibu ikolojia ya wanyama na mimea.

Amezitaka Halmashauri kote nchini kwa kushirikiana na TABOA pamoja na LATRA kuhakikisha elimu ya utunzaji wa mazingira inatolewa ikiwa ni pamoja na kujenga vyoo maeneo husika ili kuepukana na adha hiyo ya uchafuzi wa Mazingira.

Katika hatua nyingine amewataka wenye viwanda kuhakikisha wanazingatia mpango wa kutunza mazingira kwenye maeneo yao ya kazi (EMP) kwa kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri wa kuhifadhi taka za viwandani na majumbani ili kutunza Mazingira.

# ZIFAHAMU ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI



Mabadiliko ya Tabianchi ni ongezeko la muda mrefu la joto la wastani la Dunia ambalo husababisha kubadilika kwa mfumo mzima wa hali ya hewa, ambao mara nyingi matokeo yake huleta athari hasi katika jamii. Athari za Mabadiliko ya Tabianchi ni pamoja na kuwepo kwa mvua za juu au chini ya wastani zinazosababisha mafuriko, ukame wa muda mrefuko, kuongezeka kwa kina cha bahari kunakosababisha kupotea kwa baadhi ya visiwa na maeneo yaliyo chini ya usawa wa bahari, Kuenea kwa matukio ya moto kwenye misitu (Moto kichaa), kuenea kwa viumbe vamizi, na kubadilika na kupotea kwa mifumo ikolojia. Pia Mabadiliko ya Tabianchi husababisha watu na mifugo kuhamahama ndani ya nchi na nchi jirani (Uganda na Rwanda) kwenda Mikoa mingine ya Magharibi na Kusini mwa Tanzania. Hali hii imesababisha migogoro ya kijamii katika maeneo husika.

Ushahidi wa Kisayansi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uko bayana na umedhihirika zaidi kwenye ongezeko la joto katika bahari na ardhi. Tanzania imeanza kushuhudia mwenendo wa ongezeko la joto la bahari na ardhi. Kwa mfano tangu mwaka 2010 hadi sasa Tanzania imeshuhudia ongezeko la nyuzi 0.6 kulinganisha na ongezeko la joto katika kipindi cha mwaka 1981 hadi 2010. Maoteo ya halijoto yanaonesha kuwa Mikoa ya kanda ya Magharibi (Kigoma, Katavi, Rukwa), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Songwe, Njombe, Ringa) na Kanda ya Kati (Dodoma) itakabiliwa na ongezeko la joto kwa zaidi ya nyuzi joto 2 kati ya mwaka 2041 hadi mwaka 2071, ikilinganishwa na mikoa mingi ya Kanda ya Mashariki inayotarajiwa kushuhudia ongezeko la joto kwa zaidi ya 10$^{0}$C (Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Pwani na Kanda ya kusini) katika kipindi hicho.

Aidha, matukio ya mvua za juu ya wastani yamekuwa yakishuhudiwa katika bonde la Ziwa Victoria linalohusisha Mikoa ya Mwanza, Kagera na Kigoma. Vilevile, mvua hizo zimekuwa zikishuhudiwa katika Maeneo ya Pwani ya Kaskazini katika Mikoa ya Unguja na Pwani ikiwemo wa Dar es Salaam. Hali hii imekuwa ikisababisha mafuriko katika maeneo hayo ambayo yanayosababisha maafa kama vile kupoteza maisha, mali, uharibifu wa miundombinu, mashamba na milipuko ya magonjwa. Kwa mfano, mwaka 2020 katika Mkoa wa Dar es Salaam mvua za juu ya wastani zilizosababisha mafuriko na kuleta athari ikiwemo vifo vya watu 12 na uharibifu wa miundombinu. Pia matukio ya mvua za chini ya wastani yanayopelekea hali ya ukame yameendelea kuongezeka kwenye maeneo mbalimbali nchini na kuathiri ustawi wa jamii, shughuli za kiuchumi na Mazingira. Aidha, athari zaidi zimehusisha kupungua kwa maji kwenye Bonde la Rufiji; Kuhama kwa watu na mifugo(Shinyanga, Mwanza na Simiyu); Vifo vya mifugo (Manyara na Simanjiro).

Katika kukabiliana na athari za changamoto za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imechukua hatua mbalimbali. Lengo likiwa ni kuimarisha uwezo wa jamii, mifumo ikolojia, na sekta za uzalishaji kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupunguza uwezekano wa kupata athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu inayohimili mawimbi ya bahari kwa kujenga kuta na kingo za bahari, kujenga mifereji ya maji ya mvua, kuchimba visima virefu, kupanda mikoko na miamba ya matumbawe, Ujenzi wa miradi mikubwa na midogo ya umeme wa maji; uimarishaji wa usambazaji wa umeme kupitia programu ya Wakala wa Nishati Vijijini Nchini (REA); matumizi ya nishati ya jua katika taa za mitaani na nyumbani.

Aidha, hatua zingine zilizofanyika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na kuanzishwa kwa Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi Tanzania; Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni; Kituo cha Taifa cha Nishati Jadidifu; kuunganisha bomba la gesi asilia kwenye kaya na viwandani jijini Dar es Salaam na Mtwara; kujenga na kuboresha miundombinu ya usafiri; kupitisha sera zinazopunguza au kukuza upunguzaji wa hewa chafu na kuongeza ufahamu; kuendesha kampeni ya kitaifa ya upandaji miti na kuanzisha mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi (Climate Change Adaptation Project).



# NEMC YAENDESHA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA MAMLAKA ZA SERIKALI KATIKA MIPAKA



*Watumishi wa mipakani wakipata elimu ya Usimamizi na Ukaguzi wa bidhaa hatarishi kutoka NEMC.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC limeendesha mafunzo ya siku mbili yahusuyo Usimamizi na Ukaguzi wa bidhaa hatarishi kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali zilizopo Mipakani.

Mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa St Gasper jijini Dodoma yalilenga kuwajengea uwezo wa namna sahihi ya kuenenda katika kuhakikisha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake katika udhibiti wa taka hatarishi inazingatiwa hasa udhibiti wa uingizwaji na usafirishaji wa bidhaa hatarishi nchini kwa maslahi mapana ya mazingira.

Mada zilizofundishwa ni pamoja na Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria katika kudhibiti taka hatarishi, Mfumo wa Kisheria wa udhibiti wa biashara ya mipakani na bidhaa zenye athari kwa mazingira, Mambo ya kimazingira ya kutilia maanani mipakani, Mfumo wa kisheria wa udhibiti wa biashara ya bidhaa ya plastiki mipakani pamoja na Mradi wa majaribio wa kupunguza taka hatarishi

Taasisi zilizoshiriki mafunzo hayo ni pamoja na TBS, Ofisi ya Makamu wa Rais, TPHPA, TRA, GCLA pamoja na Kitengo Cha Usalama wa Afya Mipakani.

---

*Inatoka Uk. 12*

## VPO NA NEMC WATEKELEZA ...

Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeweza kukamilisha utekelezaji wa shughuli zifuatazo; Kuongeza uwezo wa Mamlaka za Udhibiti katika utekelezaji wa sheria ya mazingira, Kununua sanduku la vifaa vya kupimia, mchakato wa manunuzi ya sanduku upo kwenye hatu ya awali. Kutoa mafunzo maalum kwa wafanyakazi 37 kutoka TRA, TBS, Wizara ya Afya na Kilimo kuhusu ukaguzi na udhibiti wa bidhaa zenye madhara kimazingira zinazopitishwa mipakani na miongozo ya kimataifa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa watumishi kutoka vituo vya mipakani vya Namanga na Holili/Taveta, mafunzo hayo yalifanyika kuanzia tarehe 11 - 13 Mei, 2023 katika Mkoa wa Arusha. Pia mafunzo hayohayo yalitolewa kwa wafanyakazi wa TBS, TRA, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Afya, GCLA, na Ofisi ya Rais kutoka katika mipaka ya Sirari, Mutukula na Tunduma. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Dodoma kuanzia tarehe 22-23 Mei, 2023.

Vilevile kuandaa kanzidata ya usimamizi wa taka nchini. Katika kutekeleza hili NEMC waliandaa mkutano wa wadau mabalimbali na kufanikiwa kukusanya maoni juu mahitaji ya watumiaji na muundo wa mfumo, kuweka misimbo/upangaji wa mfumo, kuupitia mfumo na kuukamilisha. Mfumo huu utasaidia kuboresha mchakato utoaji wa leseni za mazingira na kufanya ufuatiliaji wa karibu. Kutoa mafunzo kwa watumishi 30 kutoka Wizara, Idara na Wakaguzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kitengo cha Mazingira cha Polisi, Maafisa wa Mahakama, Waendesha Mashtaka wa Umma na Wakaguzi wa Mazingira kuhusu usimamizi wa mazingira. Kikao cha mafunzo kilifanyika kuanzia tarehe 14 - 15 Juni, 2023 Mkoani Dodoma. Shughuli imekamilika kwa asilimia mia moja..



*Watumishi wa Wizara na Taasisi za Serikali wakipatiwa mafunzo ya kuhusu nyenzo muhimu za utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na wataalamu kutoka NEMC Jijini Dododma.*

# RAS IRINGA AITAKA NEMC KUUTAZAMA MTO RUAHA KWA JICHO LA KIPEKEE

Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa Mhandisi Leonard Masanja amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuongeza nguvu katika kuulinda Mto Ruaha.

Mhandisi Masanja ameyasema hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa NEMC - Kanda ya Kati walipofika Ofisini kwake ambapo kwa sasa Mkoa huo unahudumiwa na NEMC Kanda ya kati badala ya Kanda ya Nyanda za juu kusini kama ilivyokuwa awali.

"Uhifadhi wa vyanzo vya maji ukiwemo Mto Ruaha unaopita katika Mbuga ya wanyama ni eneo ambalo linatakiwa liangaliwe kwa jicho la kipekee sana" Amesema Mhandisi Masanja.

Akizungumza kuhusu uharibifu unaoendelea wa vyanzo vya maji amesema Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ipo na inabidi kusimamiwa.

"Tuna vyanzo mbalimbali vya maji katika Mkoa wetu wa Iringa, lakini kutokana na ukame unaojitokeza watu huvamia maeneo ya vyanzo hivyo vya maji, kuna sheria inayoelekeza shughuli zote zifanyike umbali wa mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji, hivyo ni vizuri kuisimamia" Ameongezea Mhandisi Masanja.

Naye Afisa Mazingira wa Mkoa wa Iringa Dkt. Golyama Bahat amesema kwa mwaka 2023 Mkoa wa Iringa umefanya vizuri katika upandaji miti ambapo jumla ya miti milioni 35 imepandwa hadi kufikia mwezi Julai 2023.

"Kwa mwaka huu 2023 Iringa tumepanda miti milioni thelathini na nane, ni tofauti na mwaka jana na juzi ambapo tulikuwa tunaishia kupanda miti milioni thelathini na tano kwa hiyo suala la kupanda miti ni utamaduni wetu hapa Iringa." Alieleza Dkt. Golyama.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Kanda ya Kati wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Dkt. Careen Kahangwa ametumia fursa hii kuwakumbusha watanzania kuhusu umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira kwani ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anatunza mazingira ili kulinda afya yake na ya jamii inayomzunguka.

Pia Dkt. Careen amewakumbusha wadau wa Mazingira wanaotakiwa kulipa ada ya Mazingira kila mwaka kuhakikisha wanafanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya Mazingira ya Ada na Tozo ya Mwaka 2021 inayotokana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Mhandisi Leonard Masanja akiwa katika picha ya pamoja na timu ya Watumishi wa NEMC - Kanda ya Kati walipofika ofisini kwake kwa ajili ya kujitambulisha ambapo kwa sasa Mkoa huo unahudumiwa na NEMC Kanda ya kati badala ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kama ilivyokuwa awali.*

# NEMC KANDA YA KATI YAFANYA ZIARA YA UKAGUZI WA MAZINGIRA MKOANI SINGIDA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Kati limefanya ziara ya ukaguzi wa Mazingira katika maeneo mbalimbali yanayohusisha shughuli za uzalishaji Mkoa wa Singida.

Ziara hiyo imehusisha ukaguzi wa kawaida wa Mazingira na kuona kwa namna gani Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inatekelezwa na wadau katika maeneo ya uzalishaji hasa kwenye migodi ya madini, Viwanda mbalimbali, maghala na maeneo mengine ya uzalishaji ambayo kwa namna moja ama nyingine yanaweza kuathiri Mazingira pamoja na kutoa elimu zaidi juu ya Utunzaji wa Mazingira.

Pia wataalamu wameendelea kusisitiza wamiliki wa Viwanda, migodi ya madini, maghala na maeneo mengine ya uzalishaji kuhakikisha wanafanya Shughuli zao pasipo kuharibu Mazingira kama ambavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inavyotaka.

Katika hatua nyingine Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia ziara hiyo limewakumbusha wadau wa Mazingira wanaotakiwa kulipa ada ya Mazingira kila mwaka kuhakikisha wanafanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya Mazingira ya Ada na Tozo ya Mwaka 2021 inayotokana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

Wataalamu kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Kati wanaendelea na ziara Mkoani Singida kutembelea wadau wa Mazingira, kutoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambayo inakwenda sanjari na ukaguzi wa Mazingira katika maeneo hayo ya uzalishaji.

# NEMC YATOA HUDUMA ZA USAJILI WA MIRADI PAMOJA NA WASHAURI ELEKEZI WA MAZINGIRA KWA NJIA YA MTANDAO




*Mtaalamu wa NEMC akimsajili mshauri elekezi kwenye mtandao*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa huduma ya usajili wa washauri elekezi wa mazingira pamoja na usajili wa miradi katika maonesho ya Kimataifa ya wakulima Nanenane Mkoani Mbeya.

Akitoa huduma hiyo kwa njia ya mtandao kwa wadau wa Mazingira, Bi Suzan Chawe ambaye ni Afisa Elimu Jamii mwandamizi wa Baraza, amesema huduma hii ni fursa kwa wadau wetu wanaohitaji cheti cha mazingira na usajili wa ushauri elekezi kwani inarahisisha mchakato mzima wa upatikanaji wa cheti kinachompa fursa ya kutekeleza majukumu yake kisheria.

Amesema Baraza linasimamia miradi inayofanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa njia ya mtandao kupitia (eia.nemc.or.tz) kwani njia hii inamuwezesha mwekezaji kuanzisha mchakato wa (TAM) au ukaguzi wa Mazingira (EA) kupitia mfumo wa usimamizi wa mradi (PMS)

Ameongeza kuwa katika kusajili miradi mwekezaji anatakiwa kufungua akaunti yake, kuchagua mshauri elekezi, kujaza fomu ya usajili, kufanya uchunguzi wa kina pamoja na Baraza kufanya mapitio ya taarifa za miradi.

Nyingine ni mshauri elekezi kuwasilisha andiko lililoboreshwa kwa Baraza, Baraza kuwasilisha mapendekezo ya mradi kwa Mhe.Waziri mwenye dhamana ya mazingira, kuidhinishwa kwa ripoti ya TAM na hatua ya mwisho ni kuidhinishwa kwa mradi.

Aidha amezitaja faida za kusajiliwa kwa njia ya mtandao kuwa ni kuongeza ufanisi, kupata taarifa sahihi kutoka kwa wataalamu wa mazingira, kuboresha utunzaji kumbukumbu, kuwezesha utengano wa majukumu kati ya mshauri mwelekezi na mwekezaji pamoja na kuboresha ukusanyaji wa ada.

# FAHAMU KUHUSU KATAZO LA VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI

Moja ya vyanzo vikubwa vya uchafuzi wa Mazingira ni matumizi ya vifungashio vya plastiki ambavyo vimekuwa vikitupwa hovyo baada ya kutumika na kusambaa kila mahali hali inayopelekea Mazingira kupoteza muonekano wake mzuri wa kuvutia lakini pia kusababisha athari mbalimbali kwenye udongo na viumbe hai wakiwemo binaadamu na wanyama.

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kupitia Kanuni za kupiga Marufuku ya Matumizi ya Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2022 zinaainisha kuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha, kuuza, kusambaza, kuhifadhi na kutumia mifuko ya plastiki. Kwenda kinyume na takwa hili la kisheria itampelekea mzalishaji, muingizaji ndani ya nchi, msambazaji na mtumiaji wa mifuko hii kupata adhabu ya faini au kifungo au vyote viwili kwa pamoja.

Katazo hili ni kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo athari zinazotokana na matumizi ya mifuko hiyo. Athari hizo ni kama kuharibu rutuba ya udongo na kuondoa mbolea, kuua viumbe hai vilivyomo ardhini, kusababisha magonjwa kama vile saratani, kuziba kwa mifereji ya maji taka na kusababisha mafuriko lakini pia kuzalisha gesi sumu na kusababisha magonjwa ya hewa.

Wahenga husema hakuna jambo linalokosa mbadala hivyo kutokana na katazo hilo la kisheria, Serikali imebainisha vifungashio mbadala kwa ajili ya matumizi ya kila siku.

Mifuko hiyo mbadala ni kama vile mifuko ya karatasi, bahasha, vikapu, mifuko ya ngozi.

Sifa za vifungashio kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ni pamoja na kuwa na jina na anuani ya mzalishaji, viwe na alama ya urejeleshaji, viwe na unene usiopungua microns 30 kwa upande mmoja (single layer) au microns 60 (double layer) pande mbili, viwe na alama ya ubora inayotolewa na TBS lakini pia kifungashio kifungashe bidhaa ndipo iletwe sokoni.

Kuna faida nyingi za kutumia mifuko mbadala ikiwa ni pamoja na kulinda mazingira yetu, mifuko hii ni rafiki kwa mazingira kwani huweza kurejelezwa, hulinda afya za viumbe hai, huweza kutumika kwa kipindi kirefu na pia mifuko mbadala huoza na hivyo kutoathiri rutuba na ubora wa udongo.

Wananchi wote wana wajibu wa kutii Kanuni ya katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kuhakikisha hawauzi wala kuweka sokoni mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku, kutohifadhi wala kusambaza mifuko ya plastiki iliyokatazwa, kuhakikisha hawasafirishi mifuko ya plastiki wala kuingiza nchini, kutozalisha mifuko ya plastiki na kutotumia wala kumiliki mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Katika kuhakikisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni za Marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki ya mwaka 2022 inaeleweka na kutekelezwa nchini kote, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeendelea kutoa elimu kupitia mikutano ya adhala, mitandao ya kijamii, tovuti ya Baraza pamoja na kaguzi mbalimbali za Mazingira zinazofanyika mara kwa mara nchini kote.


Pia NEMC imeendelea kushirikiana kwa ukaribu sana na Mamlaka za Serikali za mitaa yaani Halmashauri nchini kote kuhakikisha elimu juu ya katazo hili la mifuko ya plastiki inawafikia wananchi ikiwa sanjali na utekelezaji wa Kanuni hizi.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) inaendelea kutoa rai kwa wananchi wote kuendelea kutii sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuendelea kutunza Mazingira yanayowazunguka na kuacha matumizi ya vifungashio vya plastiki kama inavyoelekezwa na kanuni za Marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki ya mwaka 2022.






Kauli ya Mazingira Yetu




Kauli ya Mazingira Yetu

# KATUNI



















UKAME
©Musa NGARANGO JR.


©Musa NGARANGO JR.



TUSITUMIE SUMU WALA MABOMU WAKATI WA KUVUA SAMAKI
BAHARI NI KITEGA UCHUMI CHETU
©Musa


KIJIJI CHETU KINA NEEMA YA CHAKULA NA MATUNDA
NI KUTOKANA NA KULINDA MAZINGIRA YETU


Agosti 24, 2023 Namba 51
NAMNA GANI TUNAWEZA KIJINUSURU?
TUSIKATE MITI HOVYO
TUSIHARIBU VYANZO VYA MAJI
©Musa NGARANGO JR.


Agosti 23, 2023 Namba 50
©Musa NGARANGO JR.


Agosti 25, 2023 Namba 52
ARDHI KAME! UHARIBIFU WA VYANZO VYA MAJI UNATUTESA
©Musa NGARANGO JR.


USITU-KATE
©Musa NGARANGO JR.




*Wasiliana nasi;*

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz


**#MazingiraYetuUhaiWetu**


Namba ya Bure: **0800110116**

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz